# KIRINYAGA COUNTY MOCK FORM 4 EXAM - 2017
# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KISWAHILI 102/1

**Swali la kwanza.**

(i) Hii ni barua rasmi kwa mhariri.

(ii) Utaratibu wa kuandika barua rasmi lazima uzingatiwe.
Baadhi ya sehemu muhimu za kuzingatiwa ni:-

(a) Anwani mbili.
(b) Kichwa / mada yaani Mint / Ku / Reje.
(c) Kianzio cha salamu kwa mfano kwa mhariri.
(d) Mwili ambapo hoja za sababu za ajira za watoto zitajadiliwa.
(e) Hitimisho ambapo anaweza kutoa mwito, matumaini, changamoto na kadhalika.
(f) Jina kamili la mwandishi na sahihi ziandikwe baada ya hitimisho.

(iii) Baadhi ya hoja zinazotarajiwa ni:

(a) Umaskini unaowafanya wengi kukosa mahitaji ya kimsingi.
(b) Uyatima – Kufiwa na wazazi na kuwaacha bila wa kuwategemea.
(c) Mazingira magumu shuleni ambayo hupelekea wao kuacha shule na kujiunga na ajira. Kwa mfano: adhabu kali.
(d) Shinikizo la rika kuwashawishi wajiunge na ajira za mapema.
(e) Matumizi ya dawa za kulevya huchochea mahitaji ya ununuzi wa dawa hizi.
(f) Kushawishiwa na waajiri kwa kuwa ajira ya watoto si ghali.
(g) Ufisadi – Viongozi kukosa kuwachukulia hatua wanaoendeleza ajira ya watoto.
(h) Changamoto kama za shule kuwa mbali huwavunja moyo wa kuendelea na masomo.
(i) Wazazi wasiojiweza (vilema) huwatuma watoto wao kufanya kazi.
(j) Hali ambapo watoto hawawezi kulalamikia hali zao huwafanya waajiri kuwapendelea.
(k) Wazazi kuwalazimisha wana wao kufanya kazi za nyumbani.

*Na hoja zingine zozote.*

***TANBIHI*.**
*Mtahiniwa atakayekosa kuwa na anwani mbili, aondolewa alama 4S baada ya kutuzwa.*

**Swali la pili.**

Ni insha ya ufafanuzi ambapo mtahiniwa lazima akubaliane na kauli aliyopewa, yaani vipakatalishi vimeleta manufaa mengi.

**Maudhui**.

Baadhi ya hoja za kuzingatiwa ni:-

(i) Mtu huweza kufanyia kazi yake popote atakako kwani inabebeka kwa urahisi.
(ii) Vinaweza kutumika nyumbani bila umeme kwani vina hifadhi ya umeme kwa muda.
(iii) Ni rahisi kusoma barua pepe kwa haraka.
(iv) Vina matumizi mengi sana kwa mfano kikotoo, kalenda, runinga n.k
(v) Ni rahisi kubebeka katika mikutano.
(vi) Vinarahisisha kazi ya watu wengi.
(vii) Vimerahisisha masomo hasa katika kuandika makala marefu.

**Tanbihi.**

(a) Atakayezingatia hasara, atakuwa amepungukiwa kimaudhui. Asipite kiwango cha D (wastani)
(b) Insha bora ni ile iliyo na hoja **5** na zaidi zilizofafanuliwa vyema.

**Swali la tatu.**

(a) Hii ni insha ya methali ambapo lazima kisa kithibitishe ukweli na methali.
(b) Methali hii inamaanisha kuwa Achekaye kilema au mtu yeyote aliye na tatatizo naye itafika wakati wake wa kupatwa na janga kama hilo.

**Matumizi.**

- Hutumika kutahadharisha wale wanaowacheka wenzao wanapokuwa na matatizo ya kwamba wakati wao utafika.
- Kisa kionyeshe hali ambapo mtu alisherekea wakati mwenzake alikuwa na shida naye baadaye apate shida.

Kisa kinaweza kudhihirisha hali zifuatazo:

(a) Mtu asherehekee mwenzake aliyefiwa naye baadaye afiliwe.
(b) Mwanafunzi amcheke mwenzake asiyefaulu katika masomo naye baadaye asifaulu katika mitihani.
(c) Tajiri amcheke maskini naye mali yake ipotee baadaye.
(d) Kiongozi awacheke au awadharau anaowatawala baadaye uongozi umtoke.
(e) Mtu mzima amdhihaki mgonjwa naye apate magonjwa baadaye.

**Tanbihi.**

1. Lazima kisa kidhihirishe pande mbili za methali.
   (i) Kucheka kilema.
   (ii) Kilema kumpata.
   Atakayezingatia upande mmoja tu atakuwa na upungufu wa maudhui na asipate kiwango cha C.
2. Atakayetunga visa vingi lakini vithimbitishe ukweli wa methali ana upungufu wa kimtindo asipite kiwango cha C.
3. Atakayekosa kutunga kisa yaani atumie mifano tu achukuliwe kuwa amepotokwa kimaudhui na awekwe katika kiwango cha D 03/20.

**Swali la nne.**

- Hii ni insha ya mdokezo ambapo lazima kisa kianze kwa mdokezo aliopewa.
- Kisa chake lazima kilingane na mdokezo huu yawezekana kuna uvamizi uliotokea.
- Kisa kiafiki hali hii ambapo anaweza kuturejesha nyuma, akaeleza uvamizi ulivyotokea Au Aendelee tu na usimulizi na kueleza yaliyofuatia baadaye.
- Hali hii inaweza kuwa;
  (i) Kutekwa nyara.
  (ii) Kuvamiwa na majambazi nyumbani.

**Tanbini:**

Endapo hataanza kwa mdokezo amepungukiwa kimtindo.

**Muhimu**.

1. Insha zote lazima zitimize urefu unaokusudiwa. Upungufu wowote utashughulikiwa kulingana na mwongozo wa kudumu.
2. Insha zote (2, 3 na 4) lazima ziwe na vichwa. Mtahiniwa akiacha kichwa achukuliwe kuwa amepungukiwa kimtindo.
3. Mtahiniwa lazima asome kwa makini mtungo wa mtahiniwa akizingatia mada na matumizi ya miongozo miwili yaani wa maswali wa na viwango ili kuiweka insha ya mwanafunzi katika kiwango chake.

**MWONGOZO WA VIWANGO.**
Karatasi hii imedhamiria kutathmini uwezo wa mtihani wa kuwasiliana na msomaji na kuwasilisha ujumbe kimaandishi, akizingatia mada aliyopewa. Mawasiliano haya yatategemea ukwasi wa lugha ya mtahiniwa. Kwa kutegemea maagizo ya swali lenyewe na umahiri wa lugha, ni lazima kutilia mkazo mtindo, mada na uwezo na mtahiniwa kufuata maagizo vilivyo.

Mtahini lazima asome insha yote ili aweze kukadiria viwango mbalimbali vilivyopendekezwa, yaani A, B, C ama D kutegemea mahali popote pale pafaapo kuikadiria insha ya mtahiniwa.

**VIWANGO MBALI MBALI**

**KIWANGO CHA D – MAKI 01 – 05.**

1. Insha ya aina hii haieleweki kwa vyovyote, ama uwezo wa mtahiniwa wa kutumia lugha ni hafifu sana hivi kwamba mtahini lazima afikirie kile anachojaribu kuandika.
2. Mtahiniwa hana uwezo wa kutumia maneno ya Kiswahili kwa njia inayofaa.
3. Lugha imevurugika, uakifishaji usiofaa na insha ina makosa ya kila aina ya kisarufi, kimaendelezo, kimtindo n.k.
4. Kujitungia swali na kulijibu.
5. Insha ya urefu wa robo ikadiriwe hapa.

**NGAZI MBALIMBALI ZA KIWANGO CHA D**

**D – (Kiwango cha chini) Maki 01 – 02.**

1. Insha haina mpangilio maalum na haieleweki kwa vyovyote vile.
2. Kujitungia swali tofauti na kulijibu.
3. Kuandika kwa lugha isiyo Kiswahili au kuchanganya ndimi.
4. Kunakili swali au maswali na kuyakariri.
5. Kunakili swali au kichwa tu.

**D (Wastabu)**

**Maki 3**

1. Mtiririko wa mawazo haupo.
2. Mtahiniwa amepotoka kimaudhui.
3. Matumizi ya lugha ni hafifu mno.
4. Kuna makosa mengi ya kila aina.

**D+ (D YA JUU) MAKI 04 - 05**

1. Insha huwa na makosa mengi ya kila aina, lakini unaweza kutambua kile ambacho mtahiniwa anajaribu kuwasilisha.
2. Hoja hazikuelezwa kikamilifu / mada haikukuzwa vilivyo.
3. Mtahiniwa hana uhakika wa matumizi ya lugha.
4. Mtahiniwa hujirudiarudia.
5. Insha itakayozingatia sura lakini ikose maudhui ikadiriwe hapa.

**KIWANGO CHA C KWA JUMLA MAKI 06 – 10.**

1. Mtahiniwa anajaribu kushughulikia mada japo hakuikuza na kuiendeleza vilivyo.
2. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe kwa njia isiyovutia / hana ubunifu wa kutosha.
3. Mtahiniwa anaakifisha sentensi vibaya.
4. Mtiririko wa mawazo unaanza kujitokeza japo kwa njia hafifu.
5. Insha ina makosa mengi ya sarufi, ya msamiati na ya tahajia (hijai)
6. Insha yenye urefu wa nusu ikadiriwe hapa.

**NGAZI MBALIMBALI ZA KIWANGO CHA C**

**C - (C YA CHINI) MAKI 06 - 07**

1. Mtahiniwa ana shinda ya kuwasilisha na kutiririsha mawazo yake.
2. Mtahiniwa hana msamiati wa kutosha wala miundo ya sentensi ifaayo.
3. Mtahiniwa anafanya makosa mengi ya sarufi, ya hijai na ya msamiati na insha haieleweki kwa urahisi.

**C WASTANI MAKI 08**

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe lakini kwa nja hafifu.
2. Dhana tofauti tofauti hazijitokezi wazi.
3. Mtahiniwa hana ubunifu wa kutosha.
4. Mtiririko wa mawazo ni hafifu na hana ufundi wa lugha unaofaa.
5. Amejaribu kuishughulikia mada aliyopewa.
6. Ana shinda ya uakifishaji.
7. Anafanya makosa mengi ya sarufi, ya hijai na ya msamiati lakini bado insha inaeleweka.

**C+ (C YA JUU) MAKI 09 - 10**

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe vizuri akizingatia mada lakini kwa njia isiyokuwa na mvuto.
2. Dhana tofauti tofauti zimejitokeza japo kwa njia hafifu.
3. Kuna mtiririko wa mawazo japo hana ufundi wa lugha unaofaa.
4. Misemo na methali zimetumika kwa njia hafifu.
5. Ana shinda ya uakifishaji.
6. Kuna makosa ya sarufi ya msamiati na ya hijai yanayoathiri mtiririko wa mawazo.

**KIWANGO CHA B KWA JUMLA MAKI 11 – 15.**

1. Katika kiwango hiki, mtahiniwa anaonyesha hali ya kuimudu lugha.
2. Mtahiniwa anatumia miundo tofautitofauti ya sentensi vizuri.
3. Mtahiniwa ana uwezo wa kutumia lugha kwa ufasaha.
4. Mada imekuzwa na kuendelezwa kikamilifu. Hoja zisipungue nne katika kiwango hiki.
5. Insha ya urefu wa robo tatu ikadiriwe katika kiwango hiki.

**NGAZI MBALIMBALI ZA KIWANGO CHA D.**

**B - (B YA CHINI) MAKI 11 - 12**

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe vizuri kwa kueleza hoja tofautitofauti akizingatia mada.
2. Mtahiniwa ana mtiririko mzuri wa mawazo.
3. Mtahiniwa anatumia mifano michache ya msamiati unaovutia.
4. Makosa yanadhihirika /  kiasi.

**B WASTANI MAKI 13**

1. Mtahiniwa anadhihirisha hali ya kuimudu lugha.
2. Mawazo yake yanadhihirike akizingatia mada.
3. Mtahiniwa anateua na kutumia mifano michache ya msamiati mwafaka.
4. Sarufi yake ni nzuri.
5. Makosa ni machache / kuna makosa machache.

**B+ (B YA JUU) MAKI 14 - 15**

1. Mawazo ya mtahiniwa yanadhihirika waziwazi.
2. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe kwa njia inayovutia na kwa urahisi akizingatia mada.
3. Mtahiniwa ana mchanganyiko mzuri wa msamiati unaovutia.
4. Sarufi yake ni nzuri.
5. Uakifishaji wake wa sentensi ni mzuri.
6. Makosa ni machache ya hapa na pale.

**KIWANGO CHA a KWA JUMLA MAKI 16 – 20.**

1. Mtahiniwa ana ubunifu wa mawazo yanayodhihirika na kutiririka akizingatia mada.
2. Mtahiniwa anadhihirisha ujuzi wa lugha yenye mnato.
3. Ana uwezo wa kutumia tamathali za usemi ili kutoa hisia zake kwa urahsi.
4. Umbuji wake unadhihirisha ukomavu na ukakamavu wake  kimawazo

5. Insha ina urefu kamili.

**NGAZI MBALIMBALI ZA KIWANGO CHA A**

**A - (A YA CHINI) MAKI 16 - 17)**

1. Mtahiniwa anadhihirisha ukomavu wa lugha.
2. Mawazo yake yanadhihirika na anaishughulikia mada kikamilifu. Hoja tano kuenda juu.
3. Ana mtiririko mzuri wa mawazo.
4. Msamiati wake ni mzuri na unavutia.
5. Sarufi yake ni nzuri.
6. Anatumia miundo tofautitofauti ya sentensi kiufundi.
7. Makosa ni nadra kupatikana.

**A WASTANI MAKI - 18**

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe vizuri kulingana na mada.
2. Anajieleza kikamilifu akitumia lugha ya mnato.
3. Anatoa hoja zilizokomaa.
4. Anatumia msamiati wa hali ya juu na unaovutia zaidi.
5. Anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi kiufundi.
6. Makosa ni nadra kupatikana.

**A+ (A YA JUU) 19 - 20**

1. Mawazo yanadhihirika zaidi na mada imeshughuliwa vilivyo.
2. Anajieleza kikamilifu akitumia lugha ya mnato.
3. Hoja zake zimekomaa na zinashawishi.
4. Msamiati wake ni wa hali juu na unavutia zaidi.
5. Sarufi yake ni nzuri zaidi.
6. Anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi, kiufundi.
7. Makosa yote kwa jumla hayazidi matano.

**VIWANGO MBALIMBALI KWA MUHTASARI.**

| KIWANGO | NGAZI | MAKI |
|---|---|---|
| A | A+ | 19 - 20 |
| | A | 18 |
| | A- | 16 - 17 |
| B | B+ | 14 - 15 |
| | B | 13 |
| | B- | 11 - 12 |
| C | C+ | 09 - 10 |
| | C | 08 |
| | C- | 06 - 07 |
| D | D+ | 04 - 05 |
| | D | 03 |
| | D- | 01-02 |

**USAHIHISHAJI NA UTUZAJI KWA JUMLA.**

Mtahini ni sharti aisome insha yote akizingatia vipengee muhimu. Vipengee hivi ni maudhui, msamiati, mtindo, sarufi na hijai.

**MAUDHUI.**

1. Maudhui ni hoja au mambo yanayozungumziwa, kuelezewa au kuhadithiwa kwa mujibu wa mada iliyoteuliwa.
2. Maudhui ndio hasa uti wa mgongo wa insha yoyote ile.
3. Ubunifu wa mtahiniwa hukisiwa kwa kutathmini uzito wa maudhui yake kulingana na mada teule.

**MSAMIATI.**

- Msamiati ni jumla ya maneno yatumiwayo katika lugha husika.
- Mtahiniwa anatarajiwa kutumia msamiati unaooana na mada teule.
- Kutegemea ukwasi wa lugha alionao, mtahiniwa anatarajiwa kuikuza mada kwa kuifinyanga lugha kiufundi.
- Ni muhimu kuelewa kwamba kutokana na maendeleo na ukuaji wa teknolojia na mawasiliano maneno mapya yanaibuka kila uchao.

**MTINDO.**

Mtindo unahusu mambo yafuatayo:

- Mpangilio wa kazi kiaya.
- Mtiririko na mshikamano wa mawazo kiaya na katika insha nzima.
- Hati nzuri na inayosomeka kwa urahisi.
- Matumizi ya tamathali za usemi, kwa mfano, methali, misemo, jazanda na kadhalika.
- Kuandika herufi vizuri kwa mfano Jj, Pp, Uu, Ww na kadhalika.
- Sura ya insha.
- Unadhifu wa kazi ya mtahiniwa.

**SARUFI.**

Sarufi ndio msingi wa lugha. Ufanisi wa mawasiliano hutegemea uwezo wa mtahiniwa wa kutunga sentensi sahihi zenye uwiano wa kisarufi. Mtahini ataonyesha makosa yote ya sarufi yaliyo katika insha anayosahihisha. Makosa ya sarufi huweza kutokea katika:

(i) Matumizi ya alama za uakifishaji.
(ii) Kutumia herufi kubwa au ndogo mahali pasipofaa.
(iii) Matumizi yasiyofaa ya ngeli na viambishi, viunganishi, nyakati, hali, vihusiano na kadhalika.
(iv) Mpangilio wa maneno katika sentensi.
(v) Mnyambuliko wa vitenzi na majina.
(vi) Kuacha neno linalohitajika au kuongeza neno lisilohitajika katika sentensi.
(vii) Matumizi ya herufi kubwa:
(a) Mwanzo wa sentensi.
(b) Majina ya pekee.
(i) Majina ya mahali, maji, nchi, mataifa na kadhalika.
(ii) Siku za juma, miezi n.k.
(iii) Mashirika, masomo, vitabu n.k.
(iv) Makabila, lugha n.k.
(v) Jina la Mungu.
(vi) Majina ya kutambulisha hasa wanyama wa kufugwa, kwa mfano yale ya mbwa – Foksi, Jak, Popi, Simba, Tomi na mangineyo.
(vii) Majina halisi ya watu k.m Maria, Rutto.

**MAKOSA YA HIJAI / TAHAJIA.**

Haya ni makosa ya maendelezo. Mtahini anashauriwa asahihishe huku akiyaonyesha yanapotokea kwa mara ya kwanza tu. Makosa ya tahajia huweza kutokea katika;

(a) Kutenganisha neno kwa mfano ‘aliye kuwa’.
(b) Kuunganisha maneno kwa mfano ‘kwasababu’.

(c) Kukata silabi visivyo afikapo pambizoni kama vile ‘ngan-o’ badala ya nga-no.
(d) Kuandika herufi isiyofaa kwa mfano ‘ongesa’ badala ya ‘ongeza’.
(e) Kuacha herufi katika neno kwa mfano ‘aliekuja’ badala ya ‘aliyekuja’.
(f) Kuongeza herufi isiyohitajika kama vile ‘piya’ badala ya ‘pia’.
(g) Kuacha alama inayotarajiwa katika herufi kama vile j, i.
(h) Kukosa kuandika kistari cha kuendelezea neno afikiapo pambizoni au kukiandika mahali pasipofaa.
(i) Kuacha ritifaa au kuiandika mahali pasipofaa, kwa mfano ngombe, ngom’be, ng’ombe, ngo’mbe n.k
(k) Kuandika tarakimu kwa mfano 27 – 08 – 2013.

**ALAMA ZA KUSAHIHISHA.**

===== Hupigwa chini ya sehemu ambapo kosa la sarufi limetokea kwa mara ya kwanza tu.
——— Hupigwa chini ya sehemu au neno ambapo kosa la hijai limetokeza kwa mara ya kwanza tu.
Hutumiwa kuonyesha hoja inapokamilikia pambizoni kushoto.
^ Hutumiwa kuonyesha kuachwa kwa neno / maneno.
Hutumiwa kuonyesha msamiati bora. Alama hii hutiwa juu ya neno lenyewe.
X Hutumiwa kuonyesha msamiati usiofa. Alama hutiwa juu ya neno lenyewe.

Maelezo mafupi yanahitajika kuhusu tuzo lililotolewa. Kila ukurasa uwe na alama ya chini katikati ili kuthibitisha kuwa mtahini ameupitia ukurasa huo.
Maelezo yaonyeshe: Urefu wa insha k.v robo, nusu, robo tatu au kamili na udhaifu wa mwanafunzi.

**UKADIRIAJI WA UREFU WA INSHA.**

| | |
|---|---|
| Maneno 9 katika kila msitari. | Ukurasa mmoja na nusu |
| Maneno 8 kaitka kila msitari. | Ukurasa mmoja na robo tatu. |
| Maneno 7 katika kila msitari. | Kurasa mbili. |
| Maneno 6 katika kila msitari. | Kurasa mbili na robo. |
| Maneno 5 katika kila msitari. | Kurasa mbili na robo tatu. |
| Maneno 4 katika kila msitari. | Kurasa tatu na robo tatu. |
| Manneo 3 katika kila msitari. | Kurasa nne na nusu. |

**JUMLA YA MANENO**.

| | | |
|---|---|---|
| Kufikia maneno | 174 | Insha robo. |
| Maneno | 175 – 274 | Insha nusu. |
| Maneno | 275 – 374 | Insha robo tatu. |
| Maneno | 375 na kuendelea | Insha kamili. |

# KIRINYAGA COUNTY MOCK FORM 4 EXAM - 2017
# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KISWAHILI 102/3

1. (a)(i) Mtiririko wa mawazo ya Mstahiki Meya.
(ii) Akiwazia maneno aliyoambiwa na Diwani III.
(iii) Wakiwa katika ofisi ya Meya.
(iv) Diwani III alikuwa ameitwa na Meya kuhusiana na nyongeza ya mishahara ya madiwani, naye diwani III akajibu kuwa uwezo wa Baraza ulikuwa mdogo na akamshauri Meya kwamba ni vizuri Pia kuangalia maslahi ya wafanyakazi, ili kuzuia mivutano zaidi.
*(al 4 x 1 = al 4)*

(b Jazanda / Istiari.
Mzizi wa vizazi vya kesho – Wanaodai mishahara kwa sasa wanafanya hivyo kwa manufaa ya vizazi vya kesho.
*(al 2 x 1 = al 2)*

(c)(i) Matumizi ya mamlaka vibaya: Meya aliunda kamati nyingi na kuwafanya madiwani waliomuunga mkono viongozi katika kamati hizo.
(ii) Ufisadi: Alinyakua ardhi na kuwapa vikaragosi wake waliouunga mkono uongozi wake mbaya.
(iii) Matumizi mabaya ya vyombo vya dola. Anatumia askari kuwafurusha wafanyikazi waliogoma.
(iv) Vitisho: Alitishia kuwafuta wafanyikazi
(v) Mapendeleo: Aliwaita madiwani waliomuunga mkono mikutanoni na kumpuuzilia mbali Diwani wa III.
(vi) Propaganda: Anatumia vyombo vya habari kutangaza mema kuhusu uongozi wake; Anaagiza kuchezwa kwa nyimbo za kizalendo.
(vii) Unafiki: Ajificha katika dini na kumwita mhubiri kumwombea na kuliombea baraza kila juma. Anadai kwamba angeacha kazi yake ili kumfuata mhubiri.
(viii) Dhihaka: Anapoarifiwa watu wanakufa na kwamba kitoto kilifia mkononi mwa Siki kutokana na njaa na ugonjwa, anasema; huyo ni mmoja tu.
(ix) Wizi: Walipanga njama ya kuuza fimbo ya Meya na kuzingizia maandamano yaliyokuwepo.
(x) Ahadi za uongo: Anadai kuwa dawa zingewasili hospitalini baada ya siku tatu. Aidha anaahidi kushughulikia matatizo ya wafanyikazi baada ya wageni kuwasili.
(xi) Utawala wa kimabavu (udikteta): haruhusu yeyote kumpinga. Anasema yeye ndiye Meya na kwamba wanaopinga kama Diwani III wangoje wakati wao.
(xii) Tenga utawale: Anamtenga Diwani III katika maamuzi muhimu ya Baraza. Madiwani waliomuunga mkono walipewa nafasi za kuongoza kamati mbalimbali.
(xiii) Sheria: Anatumia mamlaka aliopewa kuwanyamazisha wapinzani wake: Collective responsibility; Mayors Act.
(xiv) Tamasha za muziki: Aliidhinisha kuandaliwa kwa tamasha ambapo vijana wangeshindania zawadi kwa kubuni, kutunga na kucheza nyimbo; na mashindano haya kuonyeshwa katika vyombo vya habari ili kuonyesha uzalendo sio tu kwa vijana bali kwa watu wote katika kila pembe ya Cheneo.
(xv) Hongo: Aliwahonga vikaragosi wake ili waendelee kumuunga mkono: Diwani I, Diwani II pamoja na Bili.
(xvi) Vikaragosi: Anatumia Madiwani; Diwani I na Diwani II ambao ni waaminifu kuendeleza sera zake mbaya.
(xvii) Mapokezi ya Mameya ya kifahari; Alitarajia kuwapokea Mameya wageni kwa njia ya kifahari akitarajia kupokea misaada kutoka kwao.

(xviii) Alitaka kupeana kandarasi kwa njia ya mapendeleo.
(xix) Kumshauri mwanakadarasi wa awali kulishtaki baraza ili afidiwe. Baadaye amegewe sehemu ya fidia.
(xx) Anamwajiri mhazili akiwa na nia ya kumfanya kikaragosi wake.

*(al 14 x 1 = al 14)*

2.(a)(i) Mtiririko wa mawazo ya Amani alipokiona kitoto kivulana cha rafikiye Fao.
(ii) Anakumbuka jinsi alivyosimuliwa na dadake Fao, kadhia zilizompata Fao.
(iii) Amani alikuwa ameenda kutembea nyumbani kwa Fao kuwajulia hali baada ya yeye kuachiliwa huru.
(iv) Amani anapofika nyumbani kwa Fao, anakipata kitoto kivulana na kumuuliza dadake Fao ni cha nani. Mawazo haya yanamjia baada ya amani kuachiwa kitoto kichanga mlangoni pake.

*(al 4 x 1 = al 4)*

(b) Msemo: Kupigwa na kibuhuti – Kupigwa na mshangao.

*(al 2 x 1 = al 2)*

(c)(i) Watoto waliohitimu umri wa kwenda shuleni kuingizwa kwenye ajira ya mishahara duni: Imani, Bob, DJ.
(ii) Walio na vyeo au matajiri, kujihusisha kimapenzi na wasichana wa shule, hivyo kukatiza masomo yao: Mtemi na Lowela
(iii) Ukosefu wa fedha kuwafanya wanafunzi kuacha shule na kuandama mikondo mibaya ya maisha ya kihalifu: Oscar Kambona.
(iv) Wakati wa ukoloni, Waafrika wachache waliokuwa na uhusiano wa karibu na wamisheni, ndio tu Waliofaidi kupelekewa watoto wao shuleni: Babake Majisifu na Nasaba Bora.
(v) Fao, badala ya kujifanyia mtihani, anajifaidia kutokana na kuibiwa mtihani na wazazi wake.
(vi) Walimu wanaume kuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanafunzi wao na hatimaye kuwaringa: Fao na mwanafunzi wake wa kike.
(vii) Uhusiano wa kimapenzi kwa walio vyuoni: Mashaka na Ben Bella.
(viii) Ukosefu wa karo, unaowafanya wanafunzi kukatiza masomo yao na hivyo kutotimiza ndoto zao: Imani.
(ix) Walimu kukosa kuhudhuria vipindi: Mwalimu Majisifu.
(x) Wanafunzi wengine wanasingizia wenzao makosa ya uongo: Amani anawekewa karatasi cha uchochezi chumbani mwake.
(xi) Watoto wengine wanaacha shule ili wajiunge na mchezo wa kandanda: Chwechwe Makweche.
(xii) Watoto wengine wanakosa kupelekwa shule kwa vile wamelemaa: Watoto wa Majisifu.
(xiii) Wanafunzi wengine kuandama anasa na hivyo kukatiza masomo yao: Lowela.
(xiv) Watoto kutoka familia maskini kunyimwa haki ya kugharamiwa elimu yao baada ya wazazi matajiri Kujilimbikizia fedha hizi na kugharamia masomo ya watoto wao: Wazazi wa Fao.
(xv) Wanafunzi wengine wanakataa kumalizia masomo yao kutokana na kudhamini uhusiano wa kimapenzi kuliko masomo: Mashaka.

*(zozote 14 x 1 = 14)*

3. ***<u>Changamoto zinazotokana na umaskini.</u>***
(i) Ukosefu wa huduma za kimatibabu – Matuko Weye anashindwa kujitafutia matibabu ya kiakili: Aidha Chwechwe Makweche anashindwa kutafuta matibabu ili kuutibu mguu wake.
(ii) Kukatiza masomo: Mamake Imani anapatwa na kichefuchefu cha fedha hivyo hangeweza kuwalipia wanawe karo. Jambo linalomfanya Imani na Oscar Kambona kukatiza mazomo yao.
(iii) Ukosefu wa lishe – Wakiwa safarini, Amani na Imani walikosa chakula hivyo waliyala matunda mwitu. Matuko Weye hapati lishe bora.
(iv) Ukosefu wa makazi – Amani na Imani walilala vichakani kabla ya kufika Sokomoko. Matuko Weye analala mtaroni.
(v) Upikaji wa pombe haramu – Mamake Bob D.J anapika pombe haramu ili kijikimu kimaisha.

(vi) Malazi mabaya – Amani analalia kitanda cha teremko tukaze na kujifunika blanketi lililojaa mashimo.
(vii) Mishahara duni – Umaskini unawafanya Imani na Amain kukubali ajira ya mishahara duni.
(viii) Ukosefu wa mavazi – Imani alikuwa na rinda moja, Bob DJ alikuwa na kuptura moja.
(ix) Ajira ya watoto – Umaskini unawafanya watoto na umri mdogo kusaka ajira: Bob DJ, Imani, Amani.
(x) Vifo – Baada ya kitoto Uhuru kukosa kutibiwa kinaaga kwa vile hawakuwa na fedha za kwenda kusaka matibabu kwingineko.
(xi) Hali ya kutamauka – Baada ya nyumba ya Imani kuchomwa anahiari kujirusha ziwa Mawewa kwani hakuwa na kwingineko kwa kwenda.
(xii) Haki kutotekelezwa – Nasaba Bora anahongana ili Yusuf Hamadi kusingiziwa mauaji na hivyo Kufungwa kifungo cha maisha.
(xiii) Ukosefu wa nauli – Amani na Imani hawangemudu nauli hivyo, wanatembea kwa miguu kwenda Sokomoko.
(xiv) Kujiingiza katika uhalifu – Oscar Kambona na genge lake la majambazi.
(xv) Kukatiza ndoto za wasomi – Imani anakatiza ndoto yake ya kuwa daktari, mamake anapokosa fedha za kumlipia karo.
(xvi) Ukosefu wa mashamba – Watu wengi wanakuwa maskini baada ya mashamba yao kunyakuliwa.
(xvii) Utegemezi – Bob DJ kujiaminisha kwa Bw na Bi maozi kwani ndio walikuwa tegemeo lake la pekee.
(xviii) Kuwepo kwa mitaa duni – Mamake Bob DJ aliishi mtaa wa madongoporomoka na kupika pombe Haramu.
(xix) Magonjwa – Mwili wa Bob DJ hauna afya na umejaa vipele.
(xx) Makazi duni – Amani anakaa kibandani kilichojengwa na dirisha la Katoni, Bawabu za gurudumu la gari.
(xxi) Kupoteza mali – Mali ya maskini inanyakuliwa na matajiri: Shamba la mamake Imani linanyakuliwa.
(xxii) Kufutwa kazi ovyo ovyo – Wafanyikazi walioajiriwa kazi walifutwa kazi ovyo ovyo kwa kunadhifisha kasri la majinuni.
(xxiii) Kunyimwa mishahara – Wafanyakazi wanaotimuliwa na Nasaba Bora kutoka kazini.

*(zozote 20 x 1 = 20)*

4.(a) Maneno ya rafikiye mwakitawa akimwambia mwakitawa kuhusu mama mmoja ambaye amekuwa akiangalia nyumba yao kwa kutumia darubini.

*(4 x 1 = al 4)*

(b) ***<u>Matatizo ya kijamii.</u>***
(i) Uzinifu: Japo Mwatela alikuwa meoa, anahusiana kimapenzi na Kananda.
(ii) Wizi wa watoto: Mwakitawa aliibiwa kutoka kwa mamake na Mwatela.
(iii) Ukatili: Kananda aligongwa kwa jiwe na mwakitawa.
(iv) Uuzaji wa binadamu: Kananda aliuzwa na Mwatela kwa dereva wa Kongo.

*(zozote 4 x 2 = al 8)*

(c) ***<u>Mwanamke anavyosawiriwa kama kiumbe duni.</u>***
(i) Ni mwoga: Kananda anakubali kuapizwa na Mwatela asimwambie mkewe kuhusu uhusiano wao uliosababisha uja uzito wake.
(ii) Ni mwenye mapuuza: Mapenzi ya Kananda kwa mwakitawa yanamfanya asichukue tahadhari anapomtazama kupitia darubini yake.
(iii) Ni yaya: Kananda anatumiwa na Bw.na Bi. Mwatela kumlea mtoto wao Sami.
(iv) Anatumiwa kama chombo cha kukidhi ashiki ya wanaume; Mwatela alikuwa akimnyemelea Kananda wakati bibi yake hakuwako nyumbani.
(v) Ni maskini: Wazazi wake Kananda kutokana na hali yao ya umaskini, wanafurahia sana Kananda Anapopata kazi ya kuwa yaya.

*(zozote 4 x 2 = al 8)*

5. ***Mambo yanayawatumbukiza vijana katika matatizo***.

(i) Ubaguzi wa rangi: Fikirini (Damu Nyeusi)
(ii) Kutegemea maamuzi ya wazazi: Amali anakosa mume.
(iii) Woga: Kananda kutishiwa na Mwatela kisha kunyanganywa mtoto wake.
(iv) Ukatili wa wazazi: Sudi kutupwa na mamake.
(v) Umaskini / Hali ngumu ya maisha: Inamfanya Kananda kutafutiwa kazi kwa Bw. Mwatela ambako anapachikwa mimba.
(vi) Posa ya Abu kukataliwa anapoipeleka kwa mamake Zena.
(vii) Christine kupata mimba akiwa chuoni.
(viii) Shinikizo la marafiki linafanya kina Semkwa wavamiwe.
(ix) Kupuuza ushauri: Christine.
(x) Tamaa ya maisha ya hadhi: Christine: Lucy.
(xi) Ufuska na anasa: Christine.
(xii) Tabia ya kidomo na kimbelembele: Seluwa.
(xiii) Ulimbukeni wa mapenzi: Unawafanya wasichana kupata mimba wakiwa shuleni: Sela na wasichana Wenzake watatu.
(xiv) Uhafidhina – Mambo ya kuchagulia wenzi wa ndoa.
Amali; msimulizi katika hadithi ya mke wangu.

*(zozote 10 x 2 = al 20)*

6. (a) Tarbia – Shairi lina mishororo minne katika kila ubeti.
*(al 2 x 1 = al 2)*

(b) Toni.
*(al 2 x 1 = al 2)*
(i) Ushauri – anawashauri wasipende machafuko.
(ii) Sikitiko.

(c)(i) Shairi limepangwa katika beti: Lina beti saba.
(ii) Mshororo wa mwisho katika kila ubeti unajirudia rudia.
(iii) Kila ubeti umegawika katika mishororo minne.
(iv) Vina vya kati na mwisho vinafanana katika kila ubeti.
(v) Kila mshororo umegawika katika pande mbili: Ukwapi na utao.
(vi) Kila mshororo una mizani nane katika ukwapi na nane katika utao.
*(al 3 x 1 = al 3)*

(d)(i) Mtiritiko – Vina vya ukwapi na utao vinafanana katika kila beti.
(ii) Mathnawi – Limegawika katika pande mbili.
*(al 2 x 1 = al 2)*

(e) Nyumbani kwetu tunaumia mioyoni mwetu kwa sababu tuko na watu wenye mambo ya ajabu na wanaotuletea shida. Watu hawa hawasikii wanambiwayo na wana dharau. Ni lazima waadhibiwe ndipo wasonge mbele.

(f)(i) Inkisari – hawendi badala ya hawaendi.
'kisema badala ya wakisema.
(ii) Tabdila – Musome badala ya msome.
(iii) Kuboronga sarufi – wangu mfiko badala ya mfiko wangu.
*(al 3 x 1 = al 3)*

(g) mshauri
*(al 2 x 1 = al 2)*

(h)(i) Misawajiko – Badilika.
(ii) Mawi – Mabaya
*(al 2 x 1 = al 2)*

7. (a) Mathnawi – Shairi limegawika katika vipande viwili.

Mtiririko – Vina vya kati na vya mwisho vinafanana katika kila ubeti.

*(al 2 x 1 = al 2)*

(b)(i) Kila ubeti umegawika katika mishororo minne.

(ii) Kila mshororo una vipande viwili; ukwapi na utao.

(iii) Kila ubeti una vina vya kati vinavyofanana na vya mwisho vinafanana pia.

(iv) Mshororo wa mwisho katika kila ubeti unajirudia rudia.

(v) Mizani ni kumi na sita katika kila mshororo.

*(Hoja zozote 4 x 1 = al 4)*

(c)(i)(a) Ankisari – Iso – Isiyo

(b) Tabdila – miyaka – miaka

(c) Lahaja Hino – hiyo; ndio -ndio

*(zozote 3 x 1 = al 3)*

(ii)(a) Inkisari – ili kulea urari wa mizani: Iso – Isiyo.

(b) Tabdila ili kuleta mahadhi katika ushairi miyaka – miaka.

(c) Lahaja – Ili kuleta urari wa vina: Siambi – Sisemi.

*(al 3)*

(d) kushtumu: Anashtumu viongozi walio na majiambo; wanaopeana ahadi za uongo.

Kukanya: Anakanya viongozi wasiwe na majibambo; wafujaji wa pesa za umma na wenye kupeana ahadi za uongo.

*(zozote 2 x 1 = al 2)*

(e) Istiara – kwamba were ndiwe jimbi.

*(al 2 x 1 = al 2)*

Nafsi neni mpiga kura.

*(al 2 x 1 = al 2)*

Usombombi - fujo / Kusumbuliwa

Lambo - kisima cha maji / chanzo cha maji

*(al 2 x 1= al 2)*

8. (a) Ngomezi ni fasihi ya ngoma.

*(al 2 x 1= al 2)*

(b) ***<u>Udhaifu wa ngomezi.</u>***

(i) Ngoma zilipigwa na watu teule tu.

(ii) Ni vigumu kupitisha ujumbe kwa maeneo pana.

(iii) Milio ya magari na honi huweza kukanganya waliokusudiwa kupata ujumbe.

(iv) Kuwepo kwa majengo marefu ya kisasa huzuia ujumbe kuwafikia walengwa.

(v) Ndoa mseto kati ya makabila tofauti huweza kuzuia watu wengine kuelewa ujumbe unaokusudiwa.

*(zozote 4 x 1 = al 4)*

(c)(a) ***<u>Ulinganisho wa ngomezi na ngoma.</u>***

(i) Zote huwasilisha ujumbe maalum.

(ii) Kuwepo kwa ngoma.

(iii) Kuna midundo na sauti.

(iv) Watu teule hutumika kuwasilisha ujumbe.

(v) Zote ni mali ya jamii.

*(zozote 4 x 2 = al 8)*

(b) Ulinganuzi

| | Ngoma | Ngomezi |
|---|---|---|
| (i) | Huchezewa kwenye kumbi za kuigiza. | Huweza kuwasilishwa mahali popote. |

| | | |
|---|---|---|
| (ii) | Ujumbe huweza kufikia hata wasiohusika. | Ujumbe hufichika kwa wasiohusika. |
| (iii) | Huwa na wahusika wawili; wachezaji na hadhira. | Huweza kuwasilishwa na mtu mmoja aliyeteuliwa. |
| (iv) | Huwa na kunengua viungo; Miondoko ya kimwili. | Miondoko ya kimwili haishuhudiwi katika uwasilishaji wake |
| (v) | Mwasilishaji huweza kuvalia maleba. | Maleba hawa hayavaliwi katika uwasilishaji Wake |

*(zozote 3 x 2 = 6)*

# KIRINYAGA COUNTY MOCK FORM 4 EXAM - 2017

# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KISWAHILI 102/2

1. Ponografia
   Athari za ponografia
2.(1) Kuimarika kwa vyombo vya teknolojia ya habari na mawasiliano.
  (2) Makundi mbalimbali ya watu wanaobuni na kutengeneza kazi hii.
  (3) Kutosheleza ashiki mf. Kama wanamuziki wanaovutia wateja.
  *(zozote 2 x 1 = 2)*
3. Vijana huwaiga wanayoyaona na kuyasikia.
  *(al 1)*
4.(a) Vijana hushawishiwa kuingilia shughuli za ngono mapema.
  (b) Vijana huacha shule kabisa.
  (c) Picha za matusi hudumishwa katika kumbukumbu zao.
  (d) Kuibuka kwa lugha, ishara na miondoko inayohusiana na ngono.
  (e) Huandamana na maovu mengine.
  (f) Huzifanya nishai na hisia za watu kuwa butu.
  *(zozote 4 x 1 = al 4)*
5. (a) Kuongeza ufahamu wa umma kuhusu uovu wa picha hizi.
  (b) Watu wazima kuwajibika kuwalinda na kuwahimiza vijana.
  (c) Wale wenye midahalishi kutowaruhusu vijana kutazama uchafu.
  (d) Sheria izuie na kupiga marufuku utengenezaji na uenezaji wa uozo huo.
  (e) Kuchukua hatua kali dhidi ya wanaoivunja.
  *(zozote 4 x 1 = al 4)*
6. uchu – kutamani sana / mshawasha / kiu
  wasijipweteke – wasifuuze / washughulike / wamakinike
  kuwa butu – kukosa hisia / pungukiwa na hisia.
  *(al 3)*

*Adhibu makosa 6 x ½ ya tahajia yanapotokea mara ya kwanza = 3*
*Adhibu makosa 6 x ½ ya sarufi yanapotokea mara ya kwanza = al 3*

2. ***Muhtasari.***
  (a) (i) Kuwajibika kufanya kazi.
  (ii) Watie bidii.
  (iii) Wafanye kazi kwa busara, adabu njema na moyo mmoja.
  (iv) Wazidishe mazao mashambani ili wawe na chakula cha kutosha.
  (v) Wajishughulishe na biashara wasitegemee kuajiriwa tu.
  (vi) Wajishughulishe kuleta uchumi katika mikono ya wananchi wa Kenya badala ya kuwaacha wasihisike.
  (vii) Wazingatie elimu ya wote, kilimo, uchumi na amani.

(b)(i) Ukosefu wa elimu.
(ii) Kutojihusisha katika biashara.
(iii) Kutegemea ajira pekee.
(iv) Kuacha uchumi wa nchi mikononi mwa wageni.
(v) Kukosa elimu tambuzi / kuwa na elimu pumbao
(vi) Kuchagua viongozi kwa misingi ya kikabila au utajiri.
(vii) ukosefu wa ushirikiano.
(viii) Uzembe.

M a = 6
b – 6
u = 3

*Sarufi 6 x ½ = 3*
*Tahajia 6 x ½ = 3*
*Ziada ya maneno 05 = 1 al*
*10 = 1½ al*
*15 = 2 al*

3**. Matumizi ya lugha**.

(a) /t/ – Si ghuna (nyuzi za sauti hazitetemeki) hafifu ½
/d/ ni ghuna – Nyuzi za sauti hutetemeka / nzito ½
- *Akitaja ½*
- *Tofautisha ½*

*Alama ½ x 4 = 2*

(b) Mkusanyiko wa silabi au mofimu ambazo hutamkiwa au kuandikwa ili zilete maana inayofahamika. (al 1)

(c) Sikumwelewa - - kikanushi cha wakati uliopita.
Kuwatunza – kiambishi cha ngeli ya Ku.
*2 x ½ = al 2*

(d) Mkongwe –kivumishi cha jina / nomino
Hodari – kivumishi cha sifa.
*Tambua ½*
*Eleza ½*
*4 x ½ = al 2*

(e) Jua – Fahamu
- Sayari
Chua – Sugua kwa nguvu
Atunge sentensi mbili.
*(2 x 1 = 2)*

(f) Majizee haya yana majike mengi.
Mazee haya yana majike mengi.
*(al 2)*

(g) alikunja – Alikunjua
Ameanika – ameanua
*(2 x ½ = al 1)*

(h) Ni vigumu wanafunzi wasiomthamini mwalimu kufaulu katika masomo.
*(2 x ½ = al 2)*

(i) Nyatogo amesumbuliwa na mavu hawa kwa muda mrefu.
*(1 x 2 = al 2)*

(j) Mtahiniwa atunge sentensi akitumia neno ujenzi / ujengaji.
*(al 2)*

(k) Nilipofika – wakati.
Alipokuwa – mahali.

*(2 x 1 = al 2)*

(l) Neno – LI – YA
Mate – YA – YA *(2 x ½ = 1)*

✓ ✓ ✓ ✓

(m) Babake alimwambia, "Asha utakwenda shule utake usitake".
*(4 x ½ = al 2)*

(n)

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ✓ S✓ | | | | |
| KN✓ | | KT✓ | | |
| N✓ | S✓ | T✓ | KN2 | |
| | | | N✓ | V✓ |
| ✓ Mkulima | ambaye ni mzembe | amepata | hasara | kubwa. ✓ |

*12 x 1/3 = al 4*

(o) Nomino za pekee.
Vifupisho vya baadhi ya majina.
*2 x 1 = al 2*

(p) Ndiwe
Ndinyi / ndio *2 x ½ = al 1*

(q) Mkulima amepata mavuno mazuri
Amepata mavuno mazuri. } Kishazi huru
Mkulima aliyepanda wakati ufaao
aliyepanda wakati ufaao } Kishazi tegemezi.
*2 x 1 = al 2*

(r) Kuna uwezekano.
Hakuna uwezekano.
*2 x 1 = al 2*

(s) Ku kiambishi cha ngeli / kitenzi jina
ji kiambishi cha kujirejelea / kirejeshi / mtenda / mtendaji
*2 x 1 = al 2*

(t) mwalimu kitondo
mzigo kipozi
gari-Ala / kitumizi
*3 x 1 = al*
*Sarufi ½ x 6 = 3*
*Tahajia ½ x 6 = 3*

4. ***Isimu jamii.***

(a) Ni lugha kulingana na muktadha wa matumizi.
Ni matumizi ya lugha kulingana na muktadha.
*(al 2)*

(b)(1) Huwezesha watu kuficha siri zao kwa kuwatenga wale wasioelewa sajili ile.
(2) Hufidia mahitaji maalum ya mawasiliano.
(3) Huwezesha mawasiliano baina na kati ya watu hivyo kuelewana.
(4) Huwawezesha wazungumzaji kujikita katika muktadha huo kulingana na mada husika.
(5) Hurahishisha mawasiliano.
(6) Huondoa uchovu wa matumizi ya lugha sanifu.
*(4 x 2 = 8*

*Adhibu.*
*Sarufi ½ x 4 = 2*
*Tahajia ½ x 4 = 2*

*Al 4*